TANGAZO LA SERIKALI NA 1003 la Tarehe 20/11/2020

SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA,

(SURA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO ZA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA ZA MWAKA 2020

Jina

**1**. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Anwani za Makazi na Postikodi za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima za Mwaka 2020.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"barabara" ni pamoja na barabara kuu, barabara ya kawaida, njia, barabara funge, kichochoro, mzunguko, na njia za miguu ambazo hutumika kutoa anwani za makazi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Itilima;

"Kamati ya Wataalam" maana yake ni kamati iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 5;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Postikodi" maana yake ni kibainishi cha eneo au maeneo ya usambazaji wa huduma za posta, kinachoundwa na mfuatano wa tarakimu pekee au tarakimu na herufi.

Majukumu ya Halmashauri

**4**. Katika kuhamasisha na kutekeleza mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi, Halmashauri itakuwa na wajibu wa:

*Tangazo namba 1003 (Linaendelea)*

(a) kutenga maeneo kwa ajili ya mitaa au barabara;
(b) kuweka, kutambua na kufuta majina ya mitaa, sehemu na barabara;
(c) kuweka, kurekebisha, kutambua na kufuta nambari za nyumba, barabara na mitaa mara kwa mara kwa kadiri itakavyohitajika;
(d) kutunza na kulinda miundombinu yote ya anwani za makazi na Postikodi;
(e) kutunza kumbukumbu za majina, nambari za mitaa, barabara, nyumba na ramani na kuhakikisha kuwa kumbukumbu hizo zinapatikana kwa urahisi kwa taasisi za umma na wananchi; na
(f) kushirikisha sekta binafsi, kulingana na mazingira, katika kutekeleza mpango wa anwani za makazi na Postikodi.

Kamati ya Wataalam

**5**.- (1) Kutakuwa na Kamati ya Wataalam itakayoundwa na Mkurugenzi ndani ya kipindi cha miezi sita tangu kuanza kutumika kwa Sheria Ndogo hizi.

(2) Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wafuatao:
(a) Mkuu wa Idara inayohusika na Mipango Miji na Mazingira ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Mkuu wa Idara inayohusika na Ujenzi ambaye atakuwa Makamu Makamu Mwenyekiti);
(c) Afisa Ardhi wa Halmashauri;
(d) Mpima Ardhi wa Halmashauri;
(e) Msanifu wa Ramani wa Halmashauri; na
(f) Afisa Maendeleo ya Jamii au Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri;
(g) Afisa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Halmashauri;
(h) Afisa wa Posta; na
(i) Mwanasheria wa Halmashauri ambaye atakuwa ni Katibu.

Majukumu ya Kamati

**6**.- (1) Kamati ya Wataalam itakuwa na majukumu yafuatayo:

ya Wataalam

(a) kupendekeza kwa Halmashauri majina ya barabara na nambari za nyumba katika Halmashauri;

(b) kusimamia uwekaji wa vibao vya majina ya barabara na nambari za nyumba;

(c) kusahihisha, kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa vipengele vyote vya Mwongozo wa Mfumo wa Anwani ambavyo havipo katika mamlaka ya Halmashauri;

(d) kutoa notisi za ukiukwaji na hatua nyingine yoyote inayofaa kuchukuliwa kulingana na Sheria Ndogo hii;

(e) kutunza kumbukumbu za anwani zote kwa kila milki katika ramani kwenye sehemu zinazotunzwa na Halmashauri;

(f) kupendekeza mabadiliko ya anwani; na

(g) kufanya kazi nyingine zitakazoelekezwa na Halmashauri kuhusu Postikodi na Anwani za Makazi.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Wataalam itapokea miongozo kutoka kwa Halmashauri na itashirikiana na viongozi wa vijiji, vitongoji na mitaa kwa kadri itakavyokuwa.

Ushirikishwaji wa wadau

**7**. Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itashirikiana na taasisi za umma na binafsi katika:

(a) kutengeneza nguzo za alama za mitaa na vibao vya nambari za nyumba;

(b) kuweka nguzo za majina ya barabara, mitaa na vibao vya nambari za nyumba;

(c) kubandika au kuchora nambari za nyumba;

(d) uchapishaji wa daftari la orodha ya Postikodi;

(e) huduma za ushauri na usimamizi

(f) kuhifadhi na kulinda miundombinu ya Postikodi;

(g) kutoa vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mfumo wa Anwani za Makazi;

(h) kutoa mafunzo na kushiriki shughuli za kuhamasisha utumiaji wa mfumo wa Anwani za Makazi;

(i) uundaji wa hifadhi-data ya Anwani za Makazi na Postikodi;

(j) usambazaji na ugawaji wa Anwani za Makazi na Postikodi; na

(k) kuhusisha na kujumuisha mpango wa Anwani za Makazi katika mipango na miradi mingine kama vile ya ujenzi wa barabara, majengo, mazingira, usafi,na umeme.

Makosa 8. Endapo mtu yeyote-

(a) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kushiriki kutekeleza Mpango wa anwani za makazi na misimbo ya posta;

(b) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza miundo mbinu isiyo halali kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na kuweka, kutambua, na kufuta majina ya mitaa, sehemu na barabara ndani ya Halmashauri;

(c) atatoa kwa makusudi huku akijua ni kosa taarifa za uongo kwa Halmashauri;

(d) Atashindwa bila sababu za msingi kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) ataharibu kwa makusudi, ataziba, atang’oa au kufuta miundombinu ya Anwani za Makazi; na

(g) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) au adhabu zote mbili yaani faini na

kifungo.

Kufililisha kosa

9. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote kiasi kisichozidi shilingi laki mbili tu (200,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 9)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA**

HATI Na. ……..                                        Tarehe…………….

**FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA**

***(****Chini ya kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo za Anwani za Makazi na Postikodi za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima za Mwaka 2020)*

Mimi ......…………………... nakiri mbele ya …………..……. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Itilima, kwamba mnamo tarehe ….. ya Mwezi .... Mwaka …..… nilitenda kosa la kukiuka maelekezo ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Anwani za Makazi na Postikodi za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima za Mwaka 2020 na kuwa

nipo tayari kulipa kiasi cha Sh………………na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hii badala ya kushtakiwa Mahakamani.

Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni ya kweli nimeyatoa kadri ya ufahamu wangu leo tarehe……….Saini……………….

**AFISA MWIDHINIWA**

Nimepokea kiasi cha Sh……………………………… toka kwa mtajwa hapo juu na nimemkatia risiti namba…………………………………………………..

Jina: ……………………………………………

Cheo: ………………………………………….

Saini: …………………………………………..

*Tangazo namba 1003 (Linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Itilima imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima uliofanyika tarehe 08-09 mwezi mei mwaka 2019 mbele ya:-

………………………………

ELIZABETH M. GUMBO

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA**

**LS**

………………………………

MH. DAUDI M. NYALAMU

**MWENYEKITI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA**

**NAKUBALI**

……………………………….

MHE. SELEMANI S. JAFO (MB),

**WAZIRI WA NCHI – OR –TAMISEMI**

Dodoma

Tarehe 28 Septemba, 2020